# EDU SERIES 2021

## KISWAHILI DARASA LA TANO (5) Muda : Saa 1 Dakika 40

Paukwa ! _1_ ! Hapo zamani katika kijiji kimoja _2_ mzee mmoja maskini _3_ ambaye hana mbele wala _4_. Mzee huyu alikuwa na kazi ya kukata na kuchanja kuni na _5_ wenyeji wa mtaa huo. Kwa kuwa mzee _6_ aliishi mashambani, hawakuwa na wanunuzi wa kutosha. Siku _7_ biashara yake haikupata mnunuzi alilala njaa.

Mzee huyu _8_ moyo hata kwa zile siku alizolala njaa. _9_ tu kwenda mwituni kukata kuni na _10_ nyumbani. Siku moja alitoka _11_ na mapema, akaanza safari yake kama kawaida. Alienda moja kwa _12_ mpaka pale, _13_ alikata na kuchanja kuni zake ingawa tumbo lilikuwa _14_ kwa njaa alijikaza _15_ huku shoka likilia ko! Ko! Ko!

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. pakua | B. pakawa | C. palipo | D. pako |
| 2. | A. Pataishi | B. ataishi | C. paliishi | D. waliishi |
| 3. | A. hohe hahe | B. hohe hohe | C. hohe hake | D. hone hake |
| 4. | A. mbele | B. katika | C. nyuma | D. hajui |
| 5. | A. kuwauzia | B. kwauzia | C. kuwauliza | D. kuanzia |
| 6. | A. huyu | B. hao | C. huo | D. hiyo |
| 7. | A. yake | B. ambazo | C. ambalo | D. ambayo |
| 8. | A. hakuvunjika | B. kuvunjika | C. hakuvuujika | D. alivujika |
| 9. | A. Aliedelea | B. Alienda | C. Aliendelea | D. Alienda |
| 10. | A. kuleta | B. kuwaleta | C. kuileta | D. kuzileta |
| 11. | A. mapema | B. asubui | C. asubuhi | D. alasili |
| 12. | A. wawili | B. tatu | C. moja | D. wote |
| 13. | A. ambamo | B. ambapo | C. ambalo | D. ambacho |
| 14. | A. anaguruma | B. Linaguruma | C. Kinaguruma | D. inaguruma |
| 15. | A. kiume | B. mume | C. kike | D. kijana |


**<u>Fuata maagizo uliyopewa kujibu maswali 16-30</u>**

16. Tumia o-ote kwa usahihi
    Msikate mti________
    A. Wote B. wowote
    C. yote D. zote
17. Ni nini maana ya msemo huu: Kula mwata ni ____
    A. Kuwa na raha
    B. Kuoa
    C. Kupata taabu
    D. Kuchemua
18. Jibu la salamu
    Shikamoo! Ni _____
    A. mzuri B. njema
    C. marahaba D. vyema
19. Malipo ya masomo shuleni ni karo, malipo ya kusafiri ni ___
    A. fidia B. mshahara
    C. marupurupu D. nauli
20. Sentensi hii iko katika wakati gani?
    Nitakutembelea wakati wa likizo.

A. Ujao
B. Uliopo
C. Uliopita
D. Wakati timilifu

21. Akifisha sentensi hii Kumbe! Unakula nyoka____
A. : B.? C.! D. .

22. Taja umbo hili



A. Mche mraba
B. Mche mstatili
C. Duara dufu
D. Pia

23. Tumia kiulizi pi? Ulimshika kipepeo ___?
A. yupi B. kipi C. vipi D. wapi

24. Andika akisami ⅔ kwa maneno.
A. Robo mbili
B. Thuluthi
C. Thumni mbili
D. Thuluthi mbili

25. Mkoba wa mishale ni ___
A. poda B. podo
C. beti D. ala.

26. Ni kama mchanga kwenye karatasi. Hutumika kulainishia mbao zilizopigwa randa. Kifaa hiki huitwaje?____
A. randa B. tezo
C. msasa D. keekee.

27. Msimu wa mvua ndogondogo au mvua fupifupi ni ___
A. Masika B. Kipupwa
C. Mchoo D. Matlai

28. Kanusha sentensi hii Mtoto anakula
A. Mtoto hakuli
B. Mtoto hajala
C. Mtoto hatakula
D. Mtoto hali

29. Andika kwa wingi Cheti chako kina dosari
A. Vyeti vyenu vina dosari
B. Vyeti vyangu vina dosari
C. Vyeti vyetu vina dosari
D. Vyeti vyako vina dosari

30. <u>Ugali</u> ulipikwa. Neno lililopigiliwa mstari ni ___
A. Nomino
B. Kitenzi
C. Kivumishi
D. kiunganishi

**<u>Soma kisa kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40</u>**.

Hapo zamani za kale, Chawa na Nyigu walipanga kuhudhuria sherehe. Kabla ya sherehe, walionelea ni bora waoge na kujitakasa vizuri. Kwa vile hawakuwataka kujipangusa kwa taulo, walijianika juani ili wakauke. Baada ya kupumzika juani, walionelea ni heri wavae ili wasichelewe kuhudhuria sherehe. Wote walikuwa na sime. Nyigu akamwambia rafiki yake chawa amsaidie kuifunga sime yake kiunoni. Chawa akaifunga kwa nguvu karibu kukikata kiuno cha Nyigu. Alipoona wembamba wa kiuno cha mwenzake, Chawa alianza kucheka. Alicheka

akacheka hadi pua yake ikapasuka. Tangu siku hiyo, kiuno cha Nyigu kikawa chembamba nayo pua ya Chawa ikawa imepasuka.

31. Nyigu na Chawa ni aina ya :
    A. Wadudu B. Wanyama
    C. Nyuni D. Samaki
32. Kamilisha methali! Kidole kimoja hakivunji ____
    A. nyigu B. chawa
    C. samaki D. sijui
33. Chawa na Nyigu walipanga kufanya nini?
    A. Kuoga
    B. Kuimba
    C. Kufunga sime
    D. Kuhudhuria sherehe
34. Sime ni aina ya?
    A. Simu B. kisu
    C. mshipi D. bangili
35. Kwa nini Chawa alicheka sana___?
    A. Alipoona urefu wa Nyigu
    B. Alipoona ufupi wa Nyigu
    C. Alipofunga sime
    D. Alipoona wembamba wa kiuno cha Nyigu.
36. Ni nini maana ya neno "takasa" kama lilivyotumika kwenye kisa?
    A. Safisha B. Ringa
    C. Danganya D. Ogofya.
37. Kwa nini Chawa alipasuka pua?
    A. Alilia sana
    B. Aliimba
    C. Alicheka sana
    D. Alipofunga sime
38. Rafiki ni Yule ___
    A. Mrembo
    B. Anayekusaidia wakati wa shida
    C. Wa ukoo wenu
    D. Anayekupa peremende
39. Neno jingine lenye maana sawa na sherehe ni
    A. Arusi B. Hafla
    C. Mlo D. Kuimba
40. Kichwa mwafaka cha kisa hiki ni __
    A. Sherehe
    B. Wembamba wa kiuno cha Nyigu
    C. Sime
    D. Rafiki

**<u>Soma kifungu kisha ujibu maswali 41-50</u>**

Malaria ni ugonjwa unaoletwa na mbu. Hupenda kuishi mahali ambapo kuna giza ili wasionekane na kuangamizwa na binadamu. Hujitokeza wakati wa magharibi kuwashambulia watu. Mbu hutagia kwenye takataka au maji yaliyotuama – yaliyosimama. Mikebe mitupu yafaa kuharibiwa ili isiwe makaazi ya mbu.

Dalili za ugonjwa wa homa ya malaria ni kuumwa na kichwa, tumbo au mgongo, kuwa mlegevu, kupoteza hamu ya chakula na wakati mwingine kutapika.

Ni muhimu kuishi katika mazingira safi ili kujikinga na malaria. Hakikisha kuwa unalala ndani ya chandarua kisichopitisha mbu na kilichotiwa dawa ya kukinga mbu. Maji yaliyotuama sharti yaondolewe na nyasi zilizo karibu na makao yetu zikatwe.

Wanaoishi kwenye maeneo yenye malaria wanaweza kumeza tembe za kuzuia homa ya malaria. Malaria huua! Yapasa tushirikiane ili kuangamiza ugonjwa huu.

41. Maradhi ya malaria husababishwa na
    A. Wadudu
    B. Mvua
    C. Mbu
    D. Mikebe mitupu

42. Mbu huishi mahali penye giza ili ___
    A. wasionekane
    B. waonekane
    C. waondolewe
    D. washambulie watu

43. Mbu hushambulia watu wakati gani____
    A. Asubuhi
    B. Mchana
    C. Magharihi
    D. Wakati wowote

44. Mikebe mitupu huaribiwa ili___
    A. Yasiwe makaazi ya mbu
    B. Isifanye mazingira kuwa chafu
    C. Huwa haina kazi
    D. Hatujaelezwa

45. Unajikinga na malaria kwa _____
    A. Kula vizuri
    B. Kuishi kwa mazingira safi
    C. Kwenda hospitalini
    D. Kushirikiana

46. Ni zipi ambazo si dalili za malaria.
    A. Kutapika damu na kuwa mlegevu
    B. Kupoteza hamu ya chakula na kutapika.
    C. Kuumwa na tumbo na mgongo
    D. Kuumwa na kichwa na tumbo.

47. Mbu ni aina ya
    A. Mnyama
    B. Samaki
    C. Mdudu
    D. Ugonjwa

48. Maji yaliyotuama ni ____
    A. Maji yaliyokwama
    B. Maji yaliyokwamua
    C. Maji yaliyokwamka
    D. Maji yaliyokwamuliwa

49. Neno lingine la tembe ni ____
    A. Dawa
    B. Vidonge
    C. Pamba
    D. Tabibu

50. Mwisho wa kifungu, mwandishi anatoa mwito wa
    A. Kushirikiana ilikuangamiza adisani
    B. Kushirikiana ili kuangamiza mbu
    C. Kushirikiana ilikuangamiza malaria
    D. Kushirikiana ili kuangamiza waja.